KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

# Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 18, Issue 3
26th Safar 1433
20th Jan, 2012

# SHURUTI ZA HIJAAB

Na: Sheikh Muhammad Naasir ud Deen al-Albaani

**LA KWANZA:** NI LAZIMA LIFINIKE MWILI MZIMA ISIPOKUWA SEHEMU ZILIZORUHUSIWA KISHERIYA.
Amesema Allaah (سبحانه وتعالى) [tafsiri ya maneno]: **"Ewe Mtume! Waambie wake wako, na binti zako, na wanawake wa ki-Islamu (wengine - waambie), wajiteremshie uzuri nguo zao. Kufanya hivyo kutapelekea upesi wajulikane (kuwa ni watu wa heshima ili) wasiudhiwe. Na Allaah ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu."** [al-Ahzaab: 33:59]
Aya hii yaeleza waziwazi yakwamba ni wajibu kufinika pambo lote la mwanamke na wala wasionyeshe sehemu yake yoyote mbele ya wanaume wasiokuwa mahram zake ("wageni") isipokuwa kwa chenye kudhihirika pasipo kwa kusudia, katika hali ambayo hapatokuwa na dhambi juu yao iwapo wataharakisha kujifunika sehemu hizo.
Amesema al-Haafidh Ibn Katheer katika tafsiri yake: Hii ina maana yakwamba hawaruhusiwi kuonyesha sehemu zao za mapambo kwa wasiokuwa mahram zao, mbali na zile sehemu zisizowezekana kufichika. Amesema Ibn Mas'ud, kwa mfano kitambara, yaani walichokuwa wakivaa wanawake wa kiarabu, Jiguo la nje au juu lenye kufunika kila kilichovaliwa na mwanamke, isipokuwa kwa kitakacho onekana kwa chini ya Jiguo la nje. Hapana madhambi kwa mwanamke kuhusiana na hili kwa sababu ni vigumu kulificha.
**LA PILI:** LENYEWE HALIFAI KUWA NI PAMBO LA KUVUTIA. Amesema Allaah (سبحانه وتعالى) [tafsiri ya maneno]: **"... wala wasidhihirishe viungo vyao ..."** [an-Noor 24:31]. Maana ya ki-Ujumla ya aya hii inahusu pia Nguo ya nje, kwa sababu iwapo litapambwa, litawavutia wanaume kwake. Nukta hii inaungwa mkono na aya iliyoko katika Surat al-Ahzaab yenye [tafsiri ya maneno]: **"... wala wasidhihirishe viungo vyao ..."** [an-Noor 24:31]. Ahzaab (interpretation of the meaning): **"Na kaeni majumbani mwenu, wala msionyeshe mapambo yenu kama walivyokuwa wakionyesha mapambo yao wanawake wa zama za Ujahili (ujinga, ukafiri)."** [al-Ahzaab 33:33]. Vilevile imeungwa mkono na hadeeth ambayo Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliposema: "Kuna watu sampuli tatu, usiniulize mimi kuwahusu watu hao: mtu mwenye kuwacha jamaa'ah, mwenye kumu'asi kiongozi wake na akafa haliyakuwa ni 'asi, mtumwa mwanamume au mwanamke mwenye kutoroka na kisha kafa, na mwanamke ambaye mumewe hayupo nyumbani na akawa amemuacha na mahitaji yake yote, na baada ya (mumewe) kutoka akajitolea nafsi yake kuonekana na mtu yoyote. Usiwaulizie watu hao." (Imepokewa na al-Haakim, 1/119; Ahmad, 6/19; kutoka katika hadeeth ya Faddaalah bint 'Ubayd. Isnaad yake ni swaheeh inapatikana katika al-Adab al-Mufrad).
**LA TATU:** NI LAZIMA LIWE NI NENE NA WALA LISIPENYEZE MAONO ("SEE -THROUGH").
Kwa sababu haliwezi kufunika kisawasawa au vyenginevyo. Nguo zenye kupenyeza maono humfanya mwanamke awe ni kishawishi kikubwa na kuvutia. Kuhusiana na haya, Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Katika zama za mwisho za Ummah wangu, kutakuwa na wanawake wenye nguo lakini watakuwa uchi, na vitu juu ya vichwa vyao mfano wa nundu za Ngamia. Waapizeni hao, kwani wao wamelaaniwa." Hadeeth nyengine yaongezea: "Hawatoingia Peponi au hata angalau kupata harufu yake (hiyo pepo), hata kama harufu yake inaweza kutambulika kwa kiasi cha umbali kadhaa na kadhaa." (Imepokewa na Muslim kutoka kwenye riwaya ya Abu Hurairah).
Ibn 'Abd al-Barr amesema: "Alichomanisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) ni kwamba wanawake waliovaa nguo zilizoundwa na vitambara vyembamba vyenye kubainisha na wala havifichi kitu. (Wanawake hao) watakuwa wamevaa kimatamshi lakini kwa uhakika wako tupu. [Imepokewa na as-Suyooti katika Tanweer al-Hawaalik, 3/103].
**LA NNE:** NI LAZIMA LIWE PANA, NA WALA LISIKABE KIASI CHA KUELEZA JINSI VIUNGO VYA MWILI VILIVYO.
Makusudio ya kuvaa nguo ni kulinda pasitokee fitna, na hili linaweza kupatikana tu iwapo nguo zenyewe zitakuwa ni pana tena zisizogandamana na mwili. Nguo zenye kuganda kwenye mwili, hata kama zinaficha rangi ya ngozi, huwa bado zinatoa maelezo ya umbile na muundo wa mwili au sehemu yake, na kutengeneza picha kama ya kweli kwenye fahamu za wanaume. Dosari ya asili ya ufisadi au ya ualishi wa ufisadi inayopatikana hapo ni dhahiri isiyokuwa na shaka. Kwahivyo, nguo ni lazima iwe ni pana. Amesema Usaamah ibn Zayd: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alinipa mimi nguo nzito ya ki-Misri iliyokuwa ni mojawapo ya nguo alizopewa na Duhyat al-Kalbi, na mimi nikampa mke wangu aivae. Akasema, 'Mbona sikuoni ukiivaa nguo ya ki-Misri niliyokupa?' nikasema, 'Nilimpa mke wangu aivae.' Akaniambia, 'mwambie avae Jiguo zito chini yake, kwani mimi nahofia yakwamba huwenda ikaeleza maumbile ya mifupa yake." (Imepokewa na al-

YALIYOMO

SHARUTI ZA HIJAAB 1 - 2
WAISLAMU KUSUSIANA 3

Diyaa' al-Maqdisi katika al-Ahaadeeth al -Mukhtaarah, 1/442, na kutoka kwa Ahmad na al-Bayhaqi, kwa isnaad iliyo hasan).

**LA TANO:** HIJAAB HALIFAI KUFUKIZWA KWA BAKHOOR WALA KUTIWA MAFUTA MAZURI.

Kuna ahaadeeth nyingi zenye kuwakataza wanawake kutia manukato pindi wanapotoka kwenye nyumba zao. Hapa tutazitaja baadhi yake zenye isnaad swaheeh.

Abu Musa al-Ash'aree (رضي الله عنه) amesema: "Amesema Mtume ( صلى الله عليه وسلم): 'Mwanamke yoyote mwenye kujitia manukato kisha akapita baina ya watu ili wapate kuihisi harufu yake ya manukato, atakuwa huyo amezini.'"

Zaynab ath-Thaqafiyyah (رضي الله عنها) amesimulia yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Atakapotoka mmoja wenu (wanawake) kuelekea msikitini, basi na asiguse manukato yoyote."

Amesema Abu Hurairah (رضي الله عنه) yakwamba amesema Mtume ( صلى الله عليه وسلم): "Mwanamke yoyote aliyejitia manukato ya bakhoor, basi na asihudhurie swala ya 'Ishaa' na sisi."

Musa ibn Yassaar (رضي الله عنه) amesema yakwamba mwanamke mmoja alipishana na Abu Hurairah ( رضي الله عنه) na ikawa harufu yake ya manukato imetangaa kwenye hewa. Akasema, "Ewe mja-kazi wa kike wa al-Jabbaar, hivi wewe wenda msikitini?" Akajibu, "Na'am", akamwambia, "Na kwa ajili hiyo ukajitia manukato? Akasema, "Ndio." Akasema, "Rudi nyumbani ukaoge kwani nilimsikia Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisema: "Atakapotoka mwanamke kuelekea msikitini na manukato, Allaah hatokubali swala yake yoyote mpaka arudi nyumbani akaoge.'"

Ahaadeeth hizi ni za Ujumla katika kuhusisha kwake. Kama ambavyo makatazo yanavyohusisha manukato yenye kutumika kwenye mwili, vilevile inahusisha manukato yenye kutiwa kwenye nguo, haswa katika hadeeth ya tatu, ambapo bakhoor (udi) ilipotajwa, kwa sababu udi hutumiwa makhsusi kufukizia nguo. Sababu ya msimamo huu iko wazi, nayo ni kwamba manukato ya wanawake huwenda yakasababisha uchochezi wa matamaniwa yasiyostahili Vilevile, wanavyuoni wakaongeza mambo mengine chini ya anwani hii ya mambo yenye kustahiki kuepukwa na wanawake wanaotaka kwenda msikitini, kama vile nguo nzuri, mapambo ya vito yenye kudhihirika, mapambo ya kupita kiasi na msongamano na wanaume. Tizama Fat-h al-Baari 2/279.

Amesema Ibn Daqeeq al-'Eid: "Hii inaashiriya yakwamba imekatazwa kwa mwanamke atakae kwenda msikitini kujitia manukato, kwa sababu hii husababisha uchochezi wa matamaniwa ya wanaume. Haya yamesimuliwa na al-Manaawi katika Fayd al-Qadeer, katika uchambuzi wa hadeeth ya kwanza ya Abu Hurairah iliyotajwa hapo juu.

**LA SITA:** HIJAAB HALIFAI KUFANANA NA NGUO ZA WANAUME.

Imepokewa katika hadeeth iliyo swaheeh yakwamba wanawake wenye kuwaiga wanaume katika mavazi au njia nyenginezo wamelaaniwa. Zifuatazo ni baadhi ya ahaadeeth tuzijuazo:

Amesema Abu Hurairah (رضي الله عنه): "Mtume (صلى الله عليه وسلم) amemlaani mwanamume mwenye kuvaa nguo za wanawake, na mwanamke mwenye kuvaa nguo za wanaume."

Amesema Abd-Allaah ibn 'Amr: "Nilimsikiya Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisema: 'Si katika sisi, wanawake wenye kuwaiga wanaume, na wanaume wenye kuwaiga wanawake.'"

Amesema ibn 'Abbaas (رضي الله عنه): "Mtume (صلى الله عليه وسلم) amewalaani wanaume wenye kujifananisha na wanawake, na wanawake wenye kujifananisha na wanaume." Amesema, "Watupeni nje ya majumba yenu"'

Akasema: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimfukuza fulani na fulani, na 'Umar akamfukuza fulani na fulani." Kulingana na riwaya nyengine: "Mtume ( صلى الله عليه وسلم) amewalaani wanaume wenye kuwaiga wanawake na wanawake wenye kuwaiga wanaume."

Amesema Abd-Allaah ibn 'Amr: "Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): 'Watu sampuli tatu hawatoingia Peponi na Allaah hata hatowaangalia katika siku ya Kufufuliwa: 'mwenye kuwa'asi wazazi wake, mwanamke mwenye kuwaiga wanaume, na dayyuth (mwanamume asiyekuwa na wivu na mkewe au wanawake walio mahram zake)."

Ibn Abi Maleekah- aliyekuwa akiitwa 'Abd-Allaah ibn 'Ubayd-Allaah;amesema: "Aaisha (رضي الله عنها) aliambiwa, 'Jee iwapo mwanamke atavaa champali (viatu) za mwanamume?'" Akajibu: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) amewalaani wanawake wenye kujifanya kama wanaume.'"

Ahaadeeth hizi zinaashiriya waziwazi ni haramu kwa wanawake kuwaiga wanaume na kinyume chake. Haya kwa kawaida yanahusu mavazi na mas'ala mengine, mbali na hadeeth ya kwanza iliyonukuliwa hapo awali, inayohusisha mavazi peke yake.

Amesema Abu Daawud katika masaa'il Imaam Ahmad (Uk. 261): "Nilimsikiya Ahmad akiulizwa kumuhusu mwanamume aliyekuwa akimvisha mjakazi wake wa kike gwanda. Akasema: "Usimvishe nguo za kiume, usimfanye aonekane kuwa ni mume." Amesema Abu Daawud: "Nilimwambia Ahmad, Anaweza kumpa champali (viatu) za kijana avae?" Akajibu, "Laa, isipokuwa iwapo atazivaa kwa ajili ya kutawadha". Nikamwambia, "Jee kwa ajili ya mapambo? Akanijibu, "Laa". Nikamuuliza, "Anaweza kumnyoa nywele zake?", akajibu, "Laa".

**LA SABA:** HIJAAB HALIFAI KUFANANA NA NGUO ZA MWANAMKE KAFIRI.

Imeelezwa kwenye sheriya yakwamba Waislamu, sawa kwa wanaume na wanawake, hawafai kujifananisha au kuwaiga makafiri katika Ibada, sherehe, au mavazi yanayowahusu wao. Huu ni msingi muhimu wa ki-Islamu ambao siku hizi kwa bahati mbaya umepuuzwa na Waislamu wengi, hata wale wenye kujihusisha na mambo ya Uislamu na kuwalingania watu kwenye dini. Haya ni ema kutokana na ujinga wa kutoijua dini yao, au huwenda ikawa wanafuata matamaniwa yao, au kwa ajili ya kupotoka kwenye njia ya sawa, yakaunganishwa na mambo ya mila na desturi za kileo na kuwaiga makafiri wa Uropa. Hii ilikuwa ni mojawapo ya sababu za kudhoofika na kurudi nyuma kwa Waislamu, mambo yaliyowawezesha wageni wa kutoka ng'ambo kuja na kuwatawala na kuwashinda nguvu."...Hakika Allaah habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili wao yaliyomo katika nafsi zao ..." [al-Ra'd 13:11 – tafsiri ya maana yake]. Lau kama wangelijua. Inatakiwa ifahamike yakwamba kuna ushahidi mwingi ulio swaheeh kwa hukmu hizi muhimu katika Qur'an na Sunnah, na kwamba ushahidi katika Qur'an umefafanuliwa katika Sunnah, kama ilivyo kawaida yake.

**LA NANE:** HIJAAB HALIFAI KUWA NI VAZI LA KUJIFAKHIRI NA MAJIVUNO.

Ibn 'Umar (رضي الله عنه) amesema: "Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): 'Yoyote mwenye kuvaa nguo za kujifakhiri na majivuno katika dunia hii, Allaah atamvisha nguo ya utwevu katika siku ya kufufuliwa, kisha ataufanya moto uwakao umzunguke.'" (Hijaab al-Mar'ah al-Muslimah, Uk.54-67).

## SHEIKH FOWZAN ABAINISHA KUHUSU WAISLAMU KUWASUSIA WENZAO

Muulizaji kutoka Uingereza auliza: "Jee, yaruhusiwa kumsusia Muislamu mwenzako, ndugu yako Muislamu aliye Mzushi, na ni zipi shuruti za kumsusia mtu iwapo inaruhusiwa kufanya hivyo?"

Maelezo ya ziyada yametolewa suali lilipoulizwa: "Hapa Uingereza, baadhi ya ndugu wanawakata na kuwasusia ndugu zao na kuwaona wao kama wazushi, ingawaje uzushi wao si katika 'Aqeedah, bali ni katika u-Hizbiyyah na kuhusiana na makundi au mambo mengine yasiyokuwa hayo?"

Akajibu Sheikh:

Na'am, ndio inaruhusiwa kumsusia iwapo itakuwa imethubutu yakwamba yeye ni mzushi. IWAPO IMETHIBITISHWA yakwamba yeye ni mzushi! Lakini ni nani huyo atakaeujua uzushi kutoka katika Sunnah isipokuwa ni 'Ulamaa'. Ama kuwahusu wanafunzi wadogo au wenye kujidai kuwa na 'ilmu, basi wao hawajui uzushi kutokamana na Sunnah. Bali utakuta kila wenye kutafautiana na wao au wasiokubaliana na wao, basi kwao (hao wenye kuwakashifu wenzao), watakuwa ni wazushi. Hata kama wanatafautiana juu ya haki na wakawa hawa wanafunzi wadogo wa 'ilmu au wenye kujidai kuwa na 'ilmu wako kwenye makosa.

Jambo la kutafakari hapa si kuhusu kutafautiana au u-Hizbiyyah, bali ni kuhusu kufuata Qur'an na Sunnah. (Utakapowakuta) wenye kufuata Qur'an na Sunnah wafuate. Ama kuhusu wale wenye kwenda kinyume na Qur'an na Sunnah unatakiwa ujiepushe na kuwa kando nao, lakini suala ni kwamba ni nani anaestahiki kutoa uamuzi huo? HAPANA YOYOTE asiyekuwa AHLUL-'ILM. Ama huku kila mmoja kudai yakwamba mwengine ni mzushi, bila ya sababu yoyote isipokuwa ni kwa sababu anapingana na wewe katika rai zako, basi hivi si sawa. Iwapo mutatafautiana juu ya jambo lolote, lirudisheni kwa watu wenye 'ilmu. Hao (wenye 'ilmu) wenye kuyaregesha mas'ala kwenye Qur'an na Sunnah, wao ndio wenye kubainisha kisawasawa baina ya wazushi na wale watu wa Sunnah. Kisha baada ya kuyarudisha mas'ala kwao, sisi twajua yakwamba tunayoyafanya yako juu ya umaizi na uwazi.

## MISUKOSUKO INAYOMKUMBA MWANAMKE MWENYE KUVAA HIJAAB

Matatizo yangu ni kwamba mimi nimeanza kuvaa Hijaab hivi karibuni. Katika mji wangu, kuna wanwake wachache sana wenye kuvaa hijaab na mji wangu ni mdogo sana. Mimi nimesilimu hivi karibuni na ni mwenye asili ya Muamerika mweusi. Mume wangu ni Mpakistani na tangu kuoana sasa ni miaka kadhaa. Yeye haonekani kupendezwa na ukweli yakwamba mimi ninavaa hijaab. Hapendi kutoka na mimi hadharani nikiwa nimevaa hijaab. Sasa mimi hata sijui nifanyeje … imekuwa ni vigumu kwangu kuendelea kuvaa, lakini ni jambo ambalo mimi naelewa vyema yakwamba ni lazima nivae, kwani sisi sote inatulazimu kujitengezea njia za kutufikisha peponi. Jee nifikirie kutaka talaka, kwa sababu dini yangu ni kitu kisichokuwa na machezo kwangu. Mume wangu huyu huswali msikitini siku za Ijumaa peke yake, na mimi bado ningali nimeshikilia Uislamu wangu. Tatizo hili huniliza saa zote … kwa ihsani yako."

**JAWABU:** "Alhamdulillaah.

Kwanza kabisa, tungelipenda kukupongeza kwa kupata taufiki ya uongofu kutoka kwa Allaah na ukasilimu, dini ya kweli na ya mwisho. Namuomba Allaah atusaidie sisi na wewe katika kushikamana nayo dini hii mpaka siku ya kufa kwetu.

Mimi nakupa bishara njema ya maneno ambayo Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliyowaambia maswahaba: "Kutakuja wakati ambapo subra itakapohitajika na Yule aliyeshika (Uislamu), naye atalipwa malipo ya watu hamsini kama nyinyi." wakasema (Maswahaba), "Hamsini miongoni mwao?" Akajibu, "Laa, miongoni mwenu." [yamepokewa na ibn Naaser; yakaorodheshwa kuwa swaheeh na al-Albaani katika silsilat as-Swaheeha, 949].

Kabla hujafikiria mas'ala ya talaka, hebu jaribu kuchukuwa hatamu za daa'iyah (mlinganizi wa kike), uwalinganie mumeo na waliokuzunguka wewe kwenye Uislamu. Jambo hili litawafaidisha wengine na kukusaidia wewe mwenyewe kuwa na msimamo mzuri. Una mfano wa hilo kutoka kwa wanawake waumini waliotutangulia kama vile Umm al-Mu'mineen (Mama yao waumini), bibi Khadijah (رضي الله عنها), aliyechukuwa juhudi kubwa katika kuutuliza moyo wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) ubaki juu ya msimamo na wala usiyumbe wakati alipoanza kazi yake.

Kila alipokuwa akimtaja baada ya kufa kwake, alikuwa akimsifu kwa matamshi yenye kung'ara, kama ilivyopokewa kutoka kwa 'Aaisha (رضي الله عنها) aliyesema: "Siku moja Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimtaja Khadijah, na akamsifu sana." (Musnad al-Imam Ahmad, 24684; ikaorodheshwa kuwa hasan na al-Haythami katika al-Majma').

Mfano mwengine ni Umm-Sulaym (رضي الله عنها). Abu Twalha [ambaye kwa wakati huo alikuwa hajasilimu] alimpelekea posa kutaka kumuowa, nae akasema: "Wallaahi, Ewe Abu Twalha, mtu kama wewe hafai kukataliwa, lakini wewe ni mtu kafiri na mimi ni mwanamke Muislamu. Mimi siruhusiwi kuolewa na wewe. Lakini iwapo utasilimu, hayo ndiyo yatakayokuwa mahari yangu." Basi akasilimu na hayo yakawa ndiyo mahari yake. [Imepokewa na an-Nasaa'i, 3341, imeorodheshwa kuwa ni swaheeh na al-Albaani katika swaheeh an-Nasaa'I 3133]. Kwahiyo anza - Allaah na akusaidie kwa kumlingania mumeo na kumshawishi kwa kila njia ajishikamanishe na Uislamu na uwajibikaji wake, kama vile swala, kuvaa hijaab n.k (na kadhaalika), hususan kwa vile yeye tayari ni Muislamu.

Kumlingania mumeo ni mojawapo ya njia zenye kumpeleka mtu Peponi. Natumai yakwamba Allaah atamuongoza mumeo kwa kupitia kwa naswaha zako njema. Vilevile muombee du'aa' kwa wingi. Iwapo baada ya muda fulani huoni maendeleo mazuri yoyote, au ukaona yakwamba unaweza kupata mtu mwengine wa kukuoa aliye bora kuliko mume huyu, basi fikiria kuhusu kuachwa (talaka). Hili ni iwapo tu mtu huyu atakuwa ni mwenye kupuuza swala kabisa, kuswali atakapo na kuacha kuswali wakati mwengine. Lakini ikiwa atakuwa amewacha kuswali kabisa hata akawa haswali peke yake pia, basi huruhusiwi kukaa nae kabisa, kwa sababu kuacha swala humpelekea mtu kwenye kumkufuru Allaah (Ukafiri). Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Ahadi iliyosimama baina yetu na makafiri ni swala, yoyote mwenye kuiwacha ni kafiri." [Imepokewa na at-Tirmidhee 2621, an-Nasaa'i 463, na wengineo. Ni riwaya iliyo swaheeh, al-Mishkaat 574]. Na akasema tena (صلى الله عليه وسلم): "Baina ya Mtu, Shirk na Kufr, kunasimama kuacha kwake kuswali." [Imepokewa na Muslim 82].

Ama wewe, basi kuwa na subira katika kushikamana na Hijaab hata kama itakuwa ni jambo zito kwako. Ni mifano mingapi itokayo kwa maswahaba inayotuonyesha yakwamba walipata shida kubwa kwa ajili ya Allaah; shida tuipatayo sisi ni sehemu ndogo

ukilinganisha na wao. Hii ni njia ya kuelekea Peponi. Kwani Moto umezungukwa na mambo yenye kustarehe na matamaniwa na Pepo imezungukwa na taabu na mashaka. Kaa ukijua yakwamba suala la Hijaab limekuwa ni zito kwako kwa sababu ni jambo jipya kwako. Iwapo utakuwa na subira na Imani, uzito huu utapotea uwende zake—inshaAllaah, na litakujakuwa ni jambo rahisi kwako na utakuja kuwa mtulivu na Hijaab yako. Utakapokumbuka malipo ya Hijaab, hilo lenye uzito litakuwa jepesi. Ukweli yakwamba wewe umevaa Hijaab, hata kama waona kuwa ni jambo zito ni alama yakwamba Imani yako ina nguvu.

Namuomba Allaah atufanye sote pamoja na wewe tushikamane katika kuifuata Dini. Aameen.

## SABABU ZA KUZIDI NA KUPUNGUA IMANI YA MTU

Na: Shaykh Muhammad ibn Saalih al-Uthaymeen

Twatamani kujua ni mambo gani yenye kuwezesha Imani kuzidi na ni mambo gani yenye kuwezesha ipungue?

Ama kuhusu mambo yenye kuifanya Imani izidi, basi ni haya yafuatayo:

**LA KWANZA:** Kumjua Allaah (سبحانه وتعالى) na Majina Yake na Sifa zake. Kwa hakika kila ilimu ya mtu katika kumjua Allaah na Majina yake na Sifa zake ikizidi, basi Imani yake huzidi bila ya shaka yoyote katika matokeo yake. Hii ndio sababu utakuta yakwamba wenye 'ilimu, wenye kujua kuhusiana na Majina na Sifa za Allaah, wengine hawayajui, utakuta yakwamba wao wana Imani yenye nguvu zaidi kuliko wengine wasiokuwa wao katika suala hili.

**LA PILI:** Kuwa na mazingatio kuhusiana na alama za Allaah, zikiwemo alama za kilimwengu na za kisheriya. Kwa hakika, kila mtu anapotafakari kuhusu alama za Allaah, ambazo ni Viumbe, Mbingu, ardhi, wana-adamu, wanyama, na wengine wasiokuwa hao, watazidi Imani zao. Allaah (سبحانه وتعالى) amesema: **"Na katika ardhi zimo (alama namna kwa namna za kuonyesha kuwepo kwa Allaah) kwa wenye yakini. Na (pia) katika nafsi zenu (pia zimo alama hizo), Je! Hamuoni?"** [adh-Dhaariyaat 20:21]

Kuna aya nyingi zenye kuthibitisha haya. Ninayomaanisha ni kwamba, aya zenye kuthibitisha yakwamba iwapo mtu atazingatia na kutafakari juu ya ulimwengu, basi matokeo yake ni kwamba imani yake itazidi.

**LA TATU:** Kujitahidi kutenda mambo mema kwa wingi, kwani kila wakati mtu anapozidi kufanya mema, imani yake itazidi, ikiwa mema hayo yanatokana na amali za ulimi au vitendo vya viungo vya mwili. Kwani, kwa hakika Dhikr (kumkumbuka kwa kumtaja Allaah) huzidisha imani kwa wingi wake (idadi atakazofanya mtu) na vilevile kwa njia inavyofanywa. Swala na Saumu (kufunga) pia, na Hajj huzidisha imani kuhusiana na idadi ya utekelezaji wake inavyofanywa, na pia kuhusu njia inayotumiwa katika utekelezaji huo. Ama kuhusu sababu za kupungua kwa imani, basi ni kinyume chake kabisa cha yaliyotajwa. Kwahiyo, ujinga katika kuyajua Majina na Sifa za Allaah zitapunguza imani ya mtu. Kwa sababu iwapo mtu hayajui Majina na Sifa za Allaah, basi atakuwa amekosa 'ilmu yake, ambayo [lau kama angelijua] maregeo yake yangelimuwezesha yeye kuzidisha imani yake.

**SABABU YA PILI:** Yakwamba mtu asiyezingatia juu ya aya za kisheriya zinazohusiana na Ulimwengu. Kwa hakika hili humsababishia imani yake kupungua, au kwa uchache kukoma kuzidi.

**LA TATU:** Kutumbukia kwenye shimo la madhambi, kwani madhambi kwa hakika yana athari kubwa kwenye moyo na kwenye imani! Hii ndiyo sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: "Mzinifu hafanyi zinaa, haliyakuwa na imani wakati anapofanya kitendo hicho."

**LA NNE:** Kuwacha utwi'ifu (kwa Allaah na Mtume wake), kwani kwa hakika kuwacha kuwa mtwi'ifu ni miongoni mwa sababu zenye kupunguza imani ya mtu. Hatahivyo, iwapo kitendo hiki Fulani cha utwi'ifu kilikuwa ni waajib, na mtu akakiwacha bila ya sababu yoyote, basi huku ni kupungua kwa imani ambako mtu hulaumiwa kwayo na huadhibiwa. Lakini iwapo si waajib, au ni waajib na mtu akaliwacha kwa sababu Fulani, basi ni upungufu wa imani, ambako mtu hatoadhibiwa kwalo. Hii ndiyo sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) akatangaza yakwamba wanawake ni wapungufu katika 'Aql (akili) na Dini, na sababu akasema ni kwamba wao wana upungufu katika DIni yao ni kwa sababu wao hawaswali wala hawafungi katika ada zao, bali wameamrishwa wasiswali wala wasifunge, lakini kwa sababu wao hawawezi kuyatenda haya (wakiwa kwenye ada zao) ambayo mtu (mwanamume) atakayokuwa na uwezo nayo, hupungua (katika Dini) kumlinganisha na mwanamume katika upande huu.

## DAMU ASILIA ZA WANAWAKE

**NA: Sheikh Muhammad Ibn Saalih Al-'Uthaymeen (رحمه الله)**

Q2: Miezi miwili baada ya kuolewa, mwanamke alianza kuona vitone vya damu baada ya kutwahirika na heidh. Jee, ataruhusiwa kuswali na kufunga, au afanyeje?

**JAWABU:** Matatizo mengi yenye kukabiliwa na heidh na mambo ya ndoa ni bahari isiyokuwa na ufuo. Baadhi ya yenye kusababisha yanahusu haya matumizi ya tembe za kuzuiya heidh na tembe za kuzuiya mimba. Zamani watu walikuwa hawapati matatizo haya mengi tuliyonayo siku hizi. Hii inasikitisha. Hukmu ya kawaida ya kukumbukwa ni kwamba kila mwanamke aliye kwenye heidh anapoona ishara zinazodhihirika za Twahara, basi huyo huwa ametwahirika. Maana yake ni "chepechepe nyeupe" yajulikanayo na wanawake. Chochote kinachotoka baada ya kutwahirika, kuanzia chepechepe za manjano, chepechepe zilizorowa, au vitone, huwa si heidh na kwahivyo havimzuii mwanamke kuswali, kufunga wala hata kujamiiyana na mumewe. Umm 'Atiyyah alisema: "Hatukuzingatia mituruziko yenye rangi ya manjano kuwa na umuhimu wowote." (Al-Bukhaari) na Abu Daawud akaongezea "baada ya kutwahirika" (kumaanisha chepechepe itokayo baada ya kutwahirika hayakuzingatiwa kuwa ni heidh). Neno la kuwatahadharisha ni kwamba wanawake wasikimbilie mpaka wawe na uhakika yakwamba wako kwenye hali ya kutwahirika, kwa sababu baadhi ya wanawake pindi wanapokuwa wamekauka, hukimbilia kuoga kabla ya kuhakikisha yakwamba wameona alama ya kutwahirika. Hii ndiyo sababu ya wake wa Maswahaba walikuwa wakipeleka vibinda vyao vya pamba kwa 'AAisha (رضي الله عنهما) nae alikuwa akiwaambia, "musifanye haraka mpaka uone mturuziko mweupe (Al-Qassah Al-Bayedaa')".

## TANGAZO LA DARSA MASJID MAZRUI

Jumatatu, Jumanne, Jumatano, Alkhamisi na Jumamosi. Darsa zote ni baina ya Maghrib na 'Ishaa'. Nyote munaalikwa kuhudhuria.